

Shiriki Ukweli Kuhusu COVID-19

Jua ukweli kuhusu ugonjwa wa virusi vya corona 2019 (COVID-19) na usaidie kukomesha uenezi wa uvumi.

Ukweli

1

Maradhi yanaweza kufanya yeyote kuwa mgonjwa bila kujali jamii au kabilia.

Watu wa asili ya Asia, pamoja na Wamarekani Wachina, hawana uwezekano wa juu wa kupata COVID-19 kuliko Mmarekani yeyote. Saidia kukomesha hofu kwa kuwasaidia watu kufahamu kuwa asili ya Asia haiongezi uwezekano wa kupata au kueneza COVID-19.

Ukweli

2

Baadhi ya watu wana uwezekano wa juu wa kupata COVID-19.

Watu ambao wamekuwa karibu sana na mtu anayefahamika kuwa na COVID-19 au watu wanaoishi ndani au hivi karibuni wamekuwa katika eneo lililo na uenezi unoaendelea wana hatari ya juu ya kugonjeka.

Ukweli

3

Mtu ambaye amekamilisha karantini au ameachiliwa kutoka kwa kutengwa hana hatari ya kuambukiza watu wengine.

Kwa maelezo ya sasa, tembelea ukurasa wa tovuti ya CDC wa ugonjwa wa virusi vya corona.

Ukweli

4

Unaweza kusaidia kukomesha COVID-19 kwa kufahamu ishara na dalili:

- Homa
- Kikohozi
- Matatizo ya kupumua Tafuta ushauri wa daktari iwapo
- Utapata dalili NA
- Umekuwa karibu sana na mtu anayefahamika kuwa na COVID-19 au ikiwa unaishi ndani au hivi karibuni umekuwa katika eneo lililo na uenezi unaoendelea wa COVID-19.

Ukweli

5

Kuna mambo rahisi unaweza kufanya ili kuweka wewe na wengine mkiwa salama.

- Osha mikono yako mara nyingi kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20, haswa baada ya kusafisha pua lako, kukohoa, au kupiga chafya; kwenda chooni; na kabla ya kula au kuandaa chakula.
- Epuka kugusa macho, pua, na mdomo wako kwa mikono isiyoshwa.
- Kaa nyumbani ukiwa mgonjwa.
- Funika kikohozi chako au unapopiga chafya kwa kutumia chachi, kisha utupe chachi hio kwenye takataka.

